**NDOTO NILIYOOTA USIKU WA KUAMKIA PASAKA YA TAREHE 01/04/2018**

**TUKIO KABLA YA NDOTO**

Mwezi mmoja kabla ya ndoto hii nilitemeblea kanisa la mchungaji mmoja ambaye ndio kwanza alikuwa ameanza huduma mahali pale. Nilikuta ana changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na vyombo vya kupazia sauti pamoja na viti. Mara baada ya ibada tulienda naye mtaani kushuhudia neno la Mungu maeneo yanayozunguka hilo kanisa. Kutokana na tatizo la vyombo nilishangaa kuona hata watu waliokuwa wanaishi karibu kabisa na lile kanisa hawakujua kama kulikuwa na huduma mahali pale. Tulipowauliza walisema kuna kipindi walikuwa wakisikia watu wanaimba lakini kwa sasa kupo kimya kwa hiyo walijua labda huduma imesimama. Niliposikia hivyo niliguswa sana kutafuta angalau sipika ya kucharge ili iwasaidie kupaza sauti.

Tulikubaliana na mchungaji kugawana gharama ya kununua spika nusu kwa nusu. Niliomba wafanyakazi wenzangu kuchangia chochote; waliniunga mkono nikapa kiasi Fulani cha pesa kisha nikaenda k/koo kuuliza bei ya spika. Nilipunguziwa bei kiasi kwamba nikaona kiasi kilichobaki naweza kujazilishia mwenyewe bila kumhusisha Mchungaji. Hivyo nikanunua spika. Usiku kabla ya kulala tukafanya maombi kama familia kushukuru Mungu kwa kila mtu aliyeguswa na kutoa kwa ajili ya spika lakini pia kwa jinsi alivyonipa mzigo wa kufanikisha jambo hilo. Huo ulikuwa ni usiku wa kuamkia pasaka. Nilikuwa nimepanga kesho yake ambayo ni siku ya pasaka, niende kukabidhi hiyo spika ndipo usiku huo nikapata ndoto hii.

**NDOTO YENYEWE**

Nilikuwa katika usingizi mzito usiku wa manane (nadhani mida ya 8 au 9 usiku) nasema muda huu kwa sababu baada ya kutoka katika ndoto na baada ya kuwa nimefanya maombi kwa muda niliona muda ukiwa saa kumi alfajiri.

Katika ndoto ile niliona nimepata taarifa za msiba ila sikujua aliyekuwa amefariki alikuwa ni nani japo naona nilikuwa katika majonzi makubwa sana tena sana kwa taarifa za msiba ule. Naona tuliondoka mimi na Mchungaji wangu (Kundael Matee) kwenda kwenye ule msiba. Naona kama Mchungaji alikuwa ananisindikiza lakini pia mimi na yeye tulikuwa tunatakiwa kuendesha ibada ya mazishi katika msiba ule.

Naona tulipanda basi kusafiri kwenda katika msiba ule, ilikuwa ni safari ndefu kama mwendo wa siku nzima hivi. Kutokana uzito wa habari za msiba naona kila mara nilipokuwa nikikumbuka habari za msiba ule nilikuwa naishiwa nguvu nikiwa safarini na nilikuwa Napata fadhaiko kubwa sana kila mara.

Hatimaye tukafika sehemu ya msiba, tulikuta wapo watu wengi sana katika ule msiba. Wote walikuwa katika majonzi mazito sana kutokana na msiba ule. Naona tena

naishiwa nguvu kutokana na majonzi ya huo msiba. Huyo aliyefariki inaonekana alikuwa ni mtu wa watu sana kwa sababu kila aliyekuwepo katika msiba alikuwa analia kwa uchungu sana. Hakika waombolezaji walikuwa wengi sana tena sana na walikuwa wakitamuka kwamba “kwa nini Mungu achukue mtu mwenye msaada mkubwa kama huyu wakati kuna watu wauwaji, wengine wanabaka watoto wao, wengine wametelekeza wake zao, wengine wezi n.k” kiufupi walikuwa wanataja watu wenye dhambi kwamba pengine wao ndio wangestahili kufariki badala ya huyo aliyefariki ambaye anaonekana alikuwa mtu wa msaada mkubwa sana kwa watu hao.

Naona huyo mtu alikuwa tajiri sana kwa sababu hata kaburi lake lilijengwa hapo nyumbani kwake na lilikuwa limejengwa kama paa kwa juu kisha kaburi likajengwa chini yake. Mandhari ya jumla ya eneo lile yalikuwa yanaonesha alikuwa ni mtu tajiri sana lakini aliyekuwa anajali watu sana hata lile kaburi lilikuwa limejengwa kifahari mno.

Baadaye tukakaribishwa mimi na Mchungaji kuendesha ibada ya mazishi ktk msiba ule. Naona mimi nilipewa nafasi ya kwanza ktk kutoa neno. Naona huku nikiwa katika majonzi nikawambia waombolezaji kuwa “msilie kwa ajili ya huyu kwa sababu yeye amemaliza safari yake, tumebaki mimi na wewe, na hao mnaodhani kwamba wao wangestahili kufa badala ya huyu ni kwamba Mungu bado anawapa nafasi ya kutubu. Mungu hapendezwi na dhambi zao wala si kwamba Mungu hawaoni, lahasha bali Mungu anawataka watubu. Huyu ametangulia hatujui amekwenda wapi lakini sisi tunapewa nafasi nyingine ya kutubu” naona baada ya kusema maneno hayo watu waliokuwa wanalia na kutamka maneno hayo wakanyamaza kimya.

Naona gafla nikashikwa tena na majonzi ya ule msiba kisha nikaanguka chini hapo pembeni ya hilo kaburi na jeneza. Naona wakaleta godoro wakatandika hapo chini pembeni mwa hilo kaburi wakanilaza juu ya lile godoro kisha wakanifunika shuka.

Gafla nikajikuta nipo kuzimu. Lakini huku nikiwa huko kuzimu nilikuwa naona shughuli zote za mazishi zilizokuwa zikiendelea huku duniani ikiwa ni pamoja na kuona watu wanagawiwa chakula na jinsi Mchungaji alivyoendelea na ibada ya mazishi. Yani mbele yangu kulikuwa na kitu kama screen ambayo iligawanywa mara mbili ambapo kwa wakati mmoja nilikuwa naona mambo ya huko kuzimu na shughuli za mazishi huku duniani. Hii inathibitisha kuwa mara tu mwanadamu anapokata roho huwa anaingia katika ulimwengu mwingine kabisa. Huwa tunabaki na mwili tu, lakini kumbe anaweza kuona kinachoendelea huku duniani japo kwa muda mfupi tu baada ya hapo mawasiliano yake na huku duniani hukatika kabisa.

Huko kuzimu nilikutana na watu ninaowafahamu na wengine wachache nilikuwa siwafahamu. Ila wengi wao nilikuwa nawafahamu kwa sababu walikuwa ni watu wa huko kijijini waliofariki siku zilizopita na wengine wapo hai mpaka leo lakini niliwaona huko. Pengine nilioneshwa watu ambao nilikuwa nawafahamu ili kunipa uhakika

kwamba sehemu hiyo ilikuwa ni kuzimu, ningeoneshwa watu ambao siwafahamu ingekuwa vigumu kutambua mahali hapo. Nikaona sehemu ya huko ilikuwa ni ya kuogopesha mno kwa sababu hakukuwa na maji, hakuna miti yenye majani ya kijani kibichi, hakuna kivuli na kuna jua kali sana yani kama jua kali la saa nane mchana lakini linaonekana kuwaka muda wote. Nikaona ni kama sehemu yenye hali ya hewa ya nusu jangwa(semi-desert) iliyozungukwa na milima mikubwa sana.

Nikaona watu wenye kukata tamaa kwa kiasi kikubwa sana, ni vigumu sana kukwambia ili uelewe jinsi hao watu walivyokuwa wakionekana lakini itoshe tu kusema kwamba walikuwa ni watu ambao hawana tumaini na wapo hivyo siku zote na hawana tumaini kwamba ipo siku hiyo hali itawatoka. Kwa hiyo hali yao ilikuwa ni ya kuogofya sana tena sana. Hawana nguo kama tunazovaa sisi bali wamejitanda vipande vya vitambaa ambavyo vilikuwa vinaonekana kama vyeusi ambavyo vilikuwa vinafanana na rangi za ngozi zao japo sijui kama labda ni kwa sababu havijawahi kufuliwa au kama ni rangi yake tu. Hakuna mtu alikuwa na ngozi ya mng'ao wa asili kama mtu aliye hai bali ngozi zao zilikuwa zimefifia kama mtu asiye na hai. Niliona watu wa jinsia zote mbili na wenye rika tofauti tofauti lakini rika la watoto wadogo halikuwepo. Rika la umri wa vijana wanaoanza kupevuka lilikuwa na watu wengi sana kuliko watu wazima, pengine kwa sababu katika umri huo vijana wengi hujiona kama bado watoto lakini ukweli ni kwamba unakuta wanajua dhambi na wanazitenda bila kutubu. Watu wa huko Walikuwa wanakuja wananichungulia/ wananitazama kwa uoga sana kisha wanatokomea. Niliona walikuwa watu wenye wasiwasi mkubwa sana na wenye uoga mkubwa sana.

Naona nikaanza kuwahoji mambo mbali mbali na mtu mmoja ambaye sikujua ni nani ndiye alikuwa ananipa majibu. Sauti yake ilikuwa inatoka nyuma yangu ila sikuweza kugeuka nimwone alikuwa nani. Japo katika ndoto ile nilipata hisia kwamba alikuwa ni kama mama yangu mzazi ambaye alifariki mwaka 1995 kwa sababu kila alichokuwa akinijibu alikuwa anaanza kwa kuniita mwanangu (sijui kwa uhakika kabisa alikuwa ni nani).

Nikauliza swali (huwa nasikia huku kuna sehemu nzuri na mbaya, je, hiyo sehemu nzuri ipo wapi?). majibu: mwanangu, ni kweli hata sisi tunasikia kuna sehemu nzuri lakini mimi sijawhi kwenda huko; nikaoneshwa mtu ambaye wanasema ndiye kiongozi wao ambaye wanasema yeye ndiye aliwambia kuwa kuna hiyo sehemu nzuri lakini wao hawajawahi kufika huko ila huyo kiongozi wao inasemekana yeye ndo huwa anawambia na hawajui kama na yeye amewahi kufika huko au la. Nikaoneshwa milima kwa mbali sana wakasema nyuma ya hiyo milima ndipo hiyo sehemu nzuri inasemekana ipo. Nikauliza (je, huku huwa mnachagua viongozi?) majibu: mwanangu, hapana, huyo kijana (yule kiongozi) ndiye huwa anatuletea habari za sehemu mbalimbali kwa ujumla huku hatuna kiongozi. Sura ya mtu mmoja ambaye kwa sasa yupo hai na ambaye ni mtu wa karibu sana kwangu ilijitokeza mara moja na kunionesha yule kiongozi wao kisha ile

sura ikapotea. Pengine ile sura ya huyo mtu ilitaka kunionesha kuwa kiroho naye yupo huko ili nimpe habari njema atubu kwa sababu alikuwa tayari katika wokovu. Baada ya ndoto niliongea naye kuhusu jambo hilo na alikiri kuwa mambo yake hayakuwa sawa na aliahidi kufanya toba.

Nikauliza (je, mtu akija huku mdogo huwa anaongezeka kiumri?) majibu: alitokea binti Fulani akanijibu ndiyo lakini nikapinga majibu yake nikasema kule duniani mtu huzaliwa, hukua, huzeeka kisha hufa je, kama na huku ni hivyo huyo mtu akifa huwa anazikwa tena? Sauti ile ikanijibu kuwa alichonijibu yule binti siyo kweli. Mwanangu, huyo hajui; mtu akija huku anabaki na umri wake ule ule haongezeki tena. Kisha nikauliza tena (mbona watu wa huko wengi wametoka sehemu moja huko duniani? yani wengi wao walikuwa ni watu wa huko kijijini kwetu waliofariki siku zilizopita) majibu: mwanangu, inaonekana mtu huwa anashuka huko kulingana na sehemu alipofia (lakini pengine hii hali ya kuoneshwa watu ninao wafahamu ilifanyika kunidhihirishia kuwa kule lilikuwa ni eneo la kuzimu). Nikauliza tena (mtu huwa anaendaje huko?) nikapewa majibu huku nikioneshwa kwa picha. Mwanangu, Huwa tunaona kitu cheusi huko angani kinashuka na kinachukua muda mrefu sana mpaka kufika huku (nikaona picha ya mtu akishuka kutoka juu), akifika hapa huwa hana nguo na akishadondoka huwa analala hapo chini kwa muda mrefu sana huku akisikitika kwa nini amekuja huku, kisha akiamka huwa tunamgawia kitambaa cha kujifunika. Nikiwa napewa hayo maelezo huyo mtu akadondoka akalala kwa muda huku nikashuhudia jinsi alivyokuwa amefunika uso wake huku akiwa anasikitika sana. Baada ya muda akaamuka akakaa huku akiwa anatikisa kichwa chake kwa huzuni kubwa sana, kisha akanipotea machoni. Nikaona nauliza tena (mtu afanyeje ili asije huku?) majibu: wakati huu sikujibiwa na ile sauti bali jibu lilikuja moyoni mwangu moja kwa moja kwamba mtu anatakiwa atubu dhambi zake kabla hajafa ili asiende huko, akifa katika dhambi hawezi kubadilisha tena.

Kumbuka mambo yote haya nilikuwa naona kama video na huku nikiwa naona kinachoendelea kule kwenye mazishi. Kisha nikaona mtu mmoja ambaye tunasali naye hapa kanisani kwetu tena alikuwa ni mtu mwenye huduma ya maombi hapa kanisani. Aliponiona alifarijika sana kwa sababu nilikuwa na chupa ya maji. Basi mtu yule akanijia na kunisihi sana nimpe maji ya kunywa. Mimi nilikuwa mgumu kumpa maji nikwamwambia ‘unaona nina chupa moja tu ya maji na huku unaona hakuna maji sasa nikikupa na mimi yakiisha nitapata wapi mengine? Lakini aliendelea kuniomba hata nimgawie kiasi kidogo tu cha kutosha kujazaja mudomo wake kwa sababu toka aende huko hajawahi kunywa maji na ana kiu sana. Naona kiaamuwa kumpa yale maji naye akanywa kiasi kidogo tu kama alivyoomba. Alipomaliza kunywa yale maji akanishukuru sana tena sana huku akinipa mkono wa shukrani. Huyu ndugu alikuwa na huduma kubwa sana wakati napata hii ndoto, ilikuwa vigumu sana kumfikishia hizi habari. Hata nilipojaribu kumtafuta tukutane faragha ili nimfikishie huu ujumbe hakuwa tayari hivyo

sikuweza kuongea naye.

Mara tu baada ya kunishika mikono yake kunishukuru kwa kumpa maji, gafla nikashituka kutoka usingizini na ndoto ikaishia hapo. Nilikuwa na hofu kubwa sana kwa mambo ambayo niliyaona huko ila kitu pekee kilichonifariji na kusababisha nivumilie ile hali ni kwamba kwa sababu bado nipo hai bado ninayo nafasi ya kutubu na hatimaye kusamehewa. Masikitiko yangu yalikuwa yanasababishwa na fikira kwamba kama ningekuwa nilikuwa nimekufa alafu nikajikuta nilikuwa sehemu kama ile ingekuwaje?. Toka siku ile hata leo, kwangu mimi nikipata taarifa za msiba wa mtu huwa pengine sisikitiki sana kwa sababu huyo mtu amekufa, ila hofu yangu kubwa ni kwamba ameenda sehemu ipi baada ya kifo?

Jambo jingine ambalo nilionyeshwa katka ulimwengu wa Roho ni kwamba nilioneshwa kuwa maisha tunayoishi hapa duniani ni mafupi mno tena mno. Usije hata siku moja ukadhani maisha ya hapa duniani ni marefu, la hasha. **Hapa dunia tunaishi maisha ambayo ni kama maandalio tu ya kifo na pamoja na nafasi ambayo Mungu anatupa ili tutengeneze maisha yetu ya umilele (Yaani ili tuifikie toba).**

Kuna maisha baada ya kifo, ambayo ni maisha marefu mno. Sasa ikitokea mtu aende huko, hakika ni kilio na kusaga meno.

**MUNGU AKUBARIKI.**